

Somo la 4: Kupanga Huduma na Shughuli

Unaweza kufundisha somo hili katika ujumla wake au litenganishe katika sehemu fupi fupi. Tumia somo kulingana na hali ya eneo lako na mahitaji, umri, na uelewa wa urais wa akidi yako au wa darasa.

HUDUMA NA SHUGHULI ZINAWEZA KUTUSAIDIA KUMFUATA MWOKOZI

Katika ujana Wake, Yesu "akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu" ([Luka 2:52](#)). Waulize washiriki wa urais wa akidi au wa darasa kujadili kwa nini huduma na shughuli ni muhimu. Je, ni kwa jinsi gani zinaweza kutusaidia kuwa zaidi kama Mwokozi?

TUNAWEZA KUTIMIZA KAZI YA BWANA KWA KUPITIA KUPANGA KWENYE MALENGO

Waalike washiriki wa urais kurejelea kanuni zilizoorodheshwa katika Miongozo ya Huduma na Shughuli kwa Vijana. Waalike kutumia [Kipanga Huduma na Shughuli](#) ili kuwasaidia kutengeneza orodha ya huduma chache na mawazo ya shughuli yanayofuata kanuni hizo. Waombe kupanga moja ya shughuli hizo kwa undani zaidi kwa kutumia [Mpango wa Kina wa Huduma na Shughuli](#). Katika mkutano ujao wa urais, waombe warejelee shughuli ambazo wamefanya na jinsi zilivyoanikiwa, kulingana na kanuni katika Miongozo ya Huduma na Shughuli kwa Vijana.

NYENZO SAIDIZI

- Mawazo ya Huduma na Shughuli vinapatikana kwenye [ChildrenandYouth.ChurchofJesusChrist.org](#)
- *Kitabu cha Mwongozo wa Jumla: Kuhudumu katika Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho*, sura ya 20, [ChurchofJesusChrist.org](#)